MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.26: Msimu wa Kilimo 2023/24* *Tathmini ya Juni 11-20, 2024 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 21-30, 2024*

## MUHTASARI

- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao hususan mahindi na alizeti lakini pia itasaidia shughuli za uvunaji wa mpunga.
- Vipindi vya upepo mkali vinavyotarajiwa vinaweza kuathiri shughuli za uvuvi hususan kwenye ukanda wa pwani ya bahari na maziwa makuu.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNE 11-20, 2024


Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarenes) iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kusogea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikua la chini kidogo ya wastani. Hali hii iliimarisha upepo kutoka kusini na kusini mashariki na hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya ukavu na mvua nyepesi katika ukanda wa pwani pamoja na upepo mkali katika maeneo ya maziwa makuu na ukanda wa pwani.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNE 11-20, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu kwa ujumla wakati maeneo machache ya mikoa ya Kilimanjaro, Pwani, and Morogoro, Kagera, Arusha, Musoma yalipata mvua kwa siku kumi kati ya milimita 1 na 50. Hata hivyo, maeneo machache ya mkoa ya Dar es Salaam, Tanga na Visiwani Unguja yalipata mvua kiasi cha zaidi ya milimita 50 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku kumi kwa kipindi cha Juni 11-20, 2024

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNE 11-20, 2024

Katika dikadi hii, hali ya ukavu ilisaidia kukomaa kwa mazao, kukauka na pia uvunaji wa mazao hususan mahindi na alizeti.

Maeneo yanayopata mvua za Masika, mahindi yapo katika hatua ya kukomaa na kukauka.

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu, mahindi yapo katika hatua ya kukomaa na kukauka na baadhi ya wakulima hususan katika mkoa wa Mbeya, Kigoma,Rukwa, Mtwara na Tabora waliendelea na uvunaji wa zao hilo.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukomaa na kukauka na wakulima wanamalizia uvunaji wa zao hilo.

Wakulima waliendelea na uvunaji wa zao la alizeti katika mikoa ya Singida na Dodoma wakati katika mkoa wa Morogoro zao hilo lipo hatua ya kukomaa.

Ngano ipo katika hatua ya kukomaa hususan katika mikoa ya Mbeya na Njombe.

Zao la kahawa lipo katika hatua ya kukomaa hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama yalikuwa ya kutosha katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JUNE 11-20, 2024

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde kilipungua kidogo katika maeneo mengi nchini kutokana hali ya ukavu inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2024

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusogea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu.
Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuimarisha upepo kutoka kusini na kusini mashariki na hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2024,

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba), mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), pamoja na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu na vindi vya upepo mkali.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro) zinatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2024

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao yaliyokomaa hususan mahindi na alizeti lakini pia itasaidia shughuli za uvunaji wa mazao hayo. Hata hivyo, hali hii ya ukavu hususan kwa maeneo yanayopata mvua za masika inaweza kuathiri kukomaa kwa mahindi yaliyochelewa kupandwa.

Pia vipindi vya upepo mkali vinavyotarajiwa vinaweza kuathiri shughuli za uvuvi hususan kwenye ukanda wa pwani ya baharí na maziwa makuu.

Kwa ujumla, wakulima wanashauriwa kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.

Wafugaji wanashauriwa kuhifadhi majani ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi ya wakati muafaka wa kwenda kuvua kuepuka athari za hali mbaya ya hewa hususan upepo mkali na mawimbi makubwa.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2024

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kupungua kidogo kutokana na hali ya ukavu na upepo inayotarajiwa..